the pittsburgh promise

HATI TAARIFU

NINAHITAJI NINI KUSTAHIKI?

Ili kupata Ufadhili wa Kielimu wa Pittsburgh Promise, wanafunzi wanahitajika kuwa,: (1) wamesajiliwa katika Shule za Umma za Pittsburgh, au mojawapo ya shule nne zinazoendeshwa na Shirika la Shule za Umma za Pittsburgh na (2) Awe ameishi mji wa Pittsburgh (au Wilkinsburg) mfululizo , kuanzia angalau mwanzo wa daraja la tisa; (3) amehitimu kutoka kwa mojawapo ya Shule za Upili za Umma za Pittsburgh (PPS) na takribani GPA ya 2.50 na rekodi ya mahudhurio ya asilimia 90% au zaidi.

Wanafunzi waliotimiza matakwa mengine ya ustahiki wa Ufadhili huu wa Kielimu wa Promise lakini wamehitimu na jumla ya GPA ya kati ya 2.0 na 2.49 wanaweza kutuma ombi la kuwekwa kwa Programu Endelezi ya Ufadhili wa Promise katika Chuo cha Jumuiya cha Kaunti ya Allegheny.Fedha za Ufadhili wa Promise husaidia kulipia gharama za programu, na wale wanaokamilisha mtaala wa mwaka mmoja kwa mafanikio watastahiki kupata ufadhili wa Promise.

NITAPATA KIASI GANI CHA UFADHILI HUU WA KIELIMU?

Kwa madarasa ya 2018 kuendelea mbele:

Wanafunzi wanaostahiki ambao wamesajiliwa mfululizo kuanzia siku ya kwanza ya daraja la tisa wanaweza kupata hadi. $5,000 kila mwaka. ***Kiwango cha chini zaidi cha ufadhili huu wa kielimu*** **cha $1,000 kitatolewa kila mwaka kwa wanafunzi wote wanaostahiki waliosajiliwa**.

Ufadhili wa Kielimu wa Promise ni wa aina ya "last-dollar". Hii inamaanisha kuwa kiasi cha fedha cha hadi $5,000 kitaongezwa kila mwaka kwa salio la karo la mwanafunzi husika baada ya kutolewa kwa Ufadhili wa Serikali (kama vile Pell, PHEAA, na FSEOG), ufadhili mwingine wowote wa kielimu ikiwa ni pamoja na punguzio la ada, kwa kila mojawapo ya miaka minne ya elimu ya baada ya sekondari.

Ikiwa mwanafunzi aliyepokea ufadhili wa kiwango cha juu zaidi cha $5,000 atahitaji tu $3,000 kugharamia mahitaji yake yote, mwanafunzi huyo atapokea $3,000. Ikiwa mwanafunzi hatakuwa na gharama yoyote baada ya ufadhili wote aliopokea kutumika, bado atapokea ufadhili wa Promise wa kiwango cha chini zaidi cha $1,000 utakaotumiwa kulipia gharama za shule kwa busara yake.

JE FEDHA ZA UFADHILI WA KIELIMU WA PROMISE ZINAWEZA KUTUMIKA VIPI?

Kwa madarasa ya 2018 kuendelea mbele:

Ufadhili wa Kielimu wa Promise husaidia kulipia gharama zote za shule. Hii ni pamoja na karo, ada za kimasomo, makazi, chakula na vitabu.

NINAWEZA KUTUMIA UFADHILI WA KIELIMU WA PROMISE WAPI?

Wanafunzi wanaweza kusoma katika chuo au taasisi yoyote ya kibiashara au kiufundi iliyoidhinishwa katika jimbo la Pennsylvania. Programu zinapaswa kustahiki kupokea ufadhili wa serikali wa Pell. Ufadhili huu wa Promise ni wa masomo ya baada ya kiwango cha sekondari pekee na hauwezi kutumiwa kwa kozi za kiwango cha kuhitimu (graduate level). Pia ufadhili huu haugharamii elimu ya mtandaoni.

NINAWEZA KUTUMIA UFADHILI HUU KWA MUDA GANI?

Ufadhili wa Pittsburgh Promise unapaswa kutumika kwa muda wa miaka minne punde tu baada ya kukamilisha chuo kikuu.

ORODHA YA SHULE ZA UPILI **ZINAZOSTAHIKI KWA UFADHILI WA PITTSBURGH PROMISE**

City High Charter High School Hill
House Passport Academy Pittsburgh
Allderdice Pittsburgh Brashear
Pittsburgh CAPA Pittsburgh Carrick
Pittsburgh Milliones (UPrep)
Pittsburgh Obama
Pittsburgh Online Academy*
Pittsburgh Perry
Pittsburgh Sci-Tech Academy
Pittsburgh Westinghouse
The Academy Charter High School
Urban Pathways Charter High School

** Pittsburgh Online Academy ni shule ya upili ya pekee ya masomo ya mtandaoni iliyoidhinishwa kukubali wanafunzi wenye Ufadhili wa Kielimu wa Promise*

ITAKUWAJE IKIWA MATOKEO YANGU HAYAKO KATIKA MFUMO MSINGI WA SKELI YA 4.0?

Shule za Umma za Pittsburgh zina wajibu wa kuripoti taarifa ya kielimu kwa Programu ya Ufadhili wa Promise kwa kila mwanafunzi. Mshauri wako wa Maelekezo au Mpito atashirikiana na shule yako kubainisha maendeleo yako ya kielimu na kuyatafsiri kwa sababu za kubainisha ustahiki wa ufadhili wa Promise

ITAKUWAJE IKIWA KUTATOKEA MKATIZO KATIKA USAJILI, GPA, MAHUDHURIO AU SUALA LINGINE LOLOTE LINALOATHIRI USTAHIKI WANGU KUTOKANA NA HALI ZISIZOWEZA KUEPUKIKA?

Kuna utaratibu wa kutuma ombi la kuzingatiwa (Compassion Appeal) kwa wanafunzi ambao wana masuala yanayowezakuathiri uwezo wao wa kustahiki kupokea ufadhili wa Promise. Maombi hayo huwasilishwa kupitia kwa sehemu ya wanafunzi katika tovuti ya Ufadhili wa Kielimu wa Promise. Maombi hayo hushughulikiwa kulingana na Mipango ya Kibinafsi ya Kielimu (IEPs), 504s, na hali zingine za mwanafunzi zisizoweza kuepukika. Maombi hayo pia yanaweza kuwasilishwa wakati ambapo mwanafunzi amesajiliwa katika shule ya baada ya sekondari kwa wanafunzi wanaohitaji mazingatio maalum kwa sababu ya hali za kipekee.

JE NITAHAKIKISHAJE KUWA NINADUMISHA USTAHIKI NINAPOANZA SHULE YA BAADA YA SEKONDARI?

Wanafunzi wanapaswa kudumisha GPA ya angalau 2.0 na kukamilisha kiwango cha kozi zinazohitajika kama ilivyoelezwa katika shule wanayohudhuria, kwa kawaida huwa 12–16 credits. Zungumza na wahusika shuleni kwa maelezo kamili kuhusu kozi anazohitajika kufanya mwanafunzi. Maendeleo ya Kielimu yatatathminiwa na wafadhili wa Promise mwishoni mwa kila mwaka wa shule. Masomo ya muda au ya mtandaoni hayagharamiwi na Ufadhili wa Promise. *Kumb: Katika vyuo vingi vya miaka minne, wanafunzi wanapaswa kukamilisha 15 credits kila mhula ili kuhitimu kwa muda wa miaka minne.*

NITATUMAJE OMBI?

Unapokuwa katika mwaka wa mwisho wa shule ya upili, tembelea sehemu ya wanafunzi katika tovuti ya Ufadhili wa Kielimu wa Promise na ukamilishe fomu ya FERPA Release kisha uweke orodha ya shule ambazo ungependa kuhudhuria

SHULE YANGU HUPATAJE UFADHILI WA KIELIMU WA PROMISE?

Wanafunzi huorodhesha jina la shule ambayo wangependa kuhudhuria katika sehemu ya wanafunzi kwenye tovuti ya Ufadhili wa Kielimu wa Promise na wafadhili hushughulikia maombi yao. Shule hutuma hati ya kudai fedha kutoka kwa Programu ya Ufadhili ya Pittsburgh Promise ili kupokea fedha hizo. Hundi hutumwa kwa shule hiyo moja kwa moja.

JE UNA MASWALI ZAIDI? WASILIANA NASI.

412-281-7605 (Nambari ya Simu)
412-281-7638 (Faksi)
info@pittsburghpromise.org (Barua pepe)
1901 Centre Avenue, Suite 204, Pittsburgh, PA 15219 (Anwani ya Posta)

the pittsburgh promise

Jifunze zaidi kuhusu Ufadhili wa Kielimu wa Pittsburgh:
www.pittsburghpromise.org